

Msamaha (Forgiveness)

Na

John Kombo

Msamaha

Na

John Kombo

April 4, 2014

Msamaha

Msamaha ni pumziko kutoka katika akili na moyo wa aliyekosewa hisia za pumziko dhidi ya aliyekosa, hisia zipi, ikiendelea itazuia ukuwaji wa kiroho na kihisia ya yule aliyekosewa.

Yesu aliongelea kuhusu upande ambao hauna hatia aliyekumbuka kwamba mtu alikuwa akimlalamikia. Akasema, “*Ndugu yako akikukosa enenda ukamuone wewe na yeye peke yenu; akikusikia umempata nduguyo.*” (Mat. 18:15). Hii inatofautiana sana na mwanadamu. Tunataka hadi aliyekosa aje kwetu na kuomba msamaha. Wakati fulani ni vigumu na wakati haiwezi kutokea, tunaishiwa kuwapoteza ndugu zetu katika Kristo. Hapa Yesu anaongelea yule anayesababisha dhambi. (Luka 17:3), linganisha Wagalatia 6:1; 2 Thes. 3:15; Yak. 5:19-20) katika mafundisho haya ya Yesu, aliyefanyiwa dhambi anapaswa kwenda na kumuona yule aliyemkosea. Tuwe wakweli na kuuliza, “Ni mara ngapi tumekwenda na kuwaona wanaotukosa katika kanisa? Wangapi? Mungu Baba yetu yuko tayari kutusamehe dhambi zetu (Zab. 86:5), kwa nini hatuko tayari kuwasamehe wale wanaotukosea?”

Mara zote Mungu hushuka na kuwatazama wenye dhambi ili awasamehe. Biblia inasema, “*Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi. Basi zaidi sana tukiisha kuhesabiwa haki katika damu yake, tutaokolewa na ghadhabu katika yeye.*” (Rum. 5:8-9). Upendo wa Mungu unapaswa kuonyeshwa kwa kifo cha Mwana kwa wale wasio haki. Kama msalaba ulikuwa jawabu la deni ambalo Mungu alipaswa kuwalipa wale waliotunza sheria na kufanya matendo ya dhabihu, alafu kusingekuwa na dhabihu katika kulipa deni.

Mungu hapendi yeyote apotee Biblia inasema, “*Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba.*” (2 Pet. 3:9). Ndugu, na tufanye mioyo yetu ilainike na kuwa na roho ya upendo, kuwa tayari kuwasamehe wale wanaotukosea kwa kwenda kuwaona badala ya kuwasubiri waje kuomba msamaha. Kwa kufanya hivyo tutawapata ndugu zetu ambao labda wamepotea.

John Kombo Nandwa

